LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# JE, UMEANDIKA WOSIA?

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*

KIJARIDA KUHUSU

# JE, UMEANDIKA WOSIA?

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


SHUKRANI ........................................ 4

DIBAJI ........................................ 6

UTANGULIZI ........................................ 9

1. Je, Umeandika Wosia? ........................................ 11

2. Wosia ni nini? ........................................ 11

3. Kuna Umuhimu Gani Wa Kuandika Wosia? ........................................ 11

4. Nani Anaweza Kuandika Wosia? ........................................ 12

5. Wosia Unaokubalika Kisheria Ni? ........................................ 12

6. Warithi Halali Kisheria ........................................ 13

7. Hifadhi ya Wosia ........................................ 14

8. Mfano wa Wosia ........................................ 16

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Wakili Godfrey Mpandikizi, Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi

wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.
Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria

au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTANGULIZI

Mara nyingi tumezoea kushuhudia migogoro kwenye familia hasa inapotokea mmoja wa wanandoa amefariki dunia. Waathirika zaidi huwa ni wajane na watoto baada ya ndugu za marehemu kuwanyang'anya mali na kuwaacha wakitangatanga. Ndugu hao bila kujali mali ya marehemu imepatikanaje husubiri msiba unamalizika na kuanza kunyang'anya mali na hata fedha zilizopo benki.

Tabia hizi hufanywa na ndugu wanaobweteka wakisubiri ndugu zao wafe ili warithi mali zao. Kesi nyingi zimekuwa zikiibuka kutokana na wanawake kudhulumiwa mali walizochuma na wenzi wao na wakati mwingine watoto nao huwageuka mama zao kwa kuwadhulumu mali zilizochumwa na baba zao.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinawasisitiza wananchi kuona umuhimu wa kuandika wosia ili kuepusha migogoro na migongano kwenye familia inayotokea baada ya mmoja wa wanandoa kufariki dunia.

Mtu anapoandika wosia ni kitu kizuri kwa sababu yeye ndiye anayejua mali zake na mtu sahihi wa kumpa urithi huo. Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa ajili ya kukuza uelewa wa watu kuhusu umuhimu wa kuandika wosia, aina ya wosia unaokubalika kisheria, warithi halali kisheria na hata jinsi bora ya kuhifadhi wosia. Mwishoni mwa kijitabu hiki kuna mfano wa wosia ambao unaweza kumrahisishia msomaji mtiririko wa kufuata wakati wa kuandika wosia unaokubalika kisheria.

## 1. JE, UMEANDIKA WOSIA?

(Unajua kitakachotokea kwa familia na mali zako ukifariki?)

## 2. WOSIA NI NINI?

Ni tamko la mdomo au maandishi anayotoa mtu wakati wa uhai wake kuelezea jinsi anavyotaka mwili wake utendewe na mali zake zigawanywe atakapokuwa amefariki.

Wosia ni siri ambayo hufichuka wakati mtu aliyeutoa anapokuwa amefariki.

## 3. KUNA UMUHIMU GANI WA KUANDIKA WOSIA?

Unaweka mambo yako bayana kuondoa utata kwa familia na jamii yako;
Unamchagua msimamizi wa mirathi yako unayemtaka wewe;

Unatoa pia muongozo jinsi ambavyo ungependa familia yako iishi baada ya kifo chako;

Unatoa maelezo juu ya mwili na mali yako kama upendavyo wewe na kwa mujibu wa sheria.

## 4. NANI ANAWEZA KUANDIKA WOSIA?

Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi na mwenye akili timamu.

## 5. WOSIA UNAOKUBALIKA KISHERIA NI?

Wa maandishi au matamshi

Ulioshuhudiwa na watu wawili ikiwa ni wa maandishi na watu wanne ikiwa ni wa matamshi.

Ni muhimu mmoja wa mashahidi awe ndugu wa karibu ila asiwe ni mrithi

Wosia uwe ni wa mali zako binafsi na si mali za mtu mwingine

Haikubaliki mtoa wosia kumnyima mrithi halali mali bila sababu zinazokubalika kisheria.

## 6. WARITHI HALALI KISHERIA

- Mke/mume;
- Watoto wa marehemu;
- Watoto walio halalishwa kisheria;
- Wazazi na ndugu wa karibu waliokuwa wakimtegemea mtoa wosia wakati wa uhai wake.

Iwapo mwandika wosia ni mgonjwa mahututi ni muhimu ithibitishwe kuwa mtu huyo anaelewa anachokifanya na akili yake ni timamu wakati wa kuandika au kutamka wosia wake.

## 7. HIFADHI YA WOSIA

Wosia ulioandikwa unaweza kuhifadhiwa:-

- Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu;
- Kwa mwanasheria/wakili;
- Benki;
- Taasisi mbalimbali kama vile taasisi za kidini kama kanisa au msikiti;
- Kwa mtu yeyote ambaye si mrithi katika Wosia huo na anaaminika kuwa ana uwezo wa kutunza siri.

**ANGALIZO**

“Kuandika wosia si uchuro bali ni kujizatiti katika kuhakikisha mambo yako ni sawa hata usipokuwapo.”

Ni muhimu kuhakikisha kuwa Wosia unashuhudiwa na Wakili au Hakimu la sivyo wosia utakuwa hauna nguvu za kisheria na unaweza kupingwa mahakamani kuwa siyo wosia halali.

## 8. MFANO WA WOSIA

1. Huu ni wosia wangu wa mwisho mimi

   ..............................................................

   S. L. P: ................................................

2. Namchagua .....................................

   S. L. P: ................................................

   Simu: ...............................................

   Ambaye anaishi

   ..............................................................

   Kuwa msimaizi wa mirathi yangu.

3. Nitakapokufa mwili wangu ukazikwe:

   ..............................................................

   Wilaya: ............................................

   Mkoa: ...............................................

4. Mali zangu/yangu ni:

   a. ..........................................................

   b. ..........................................................

5. Natamka kwamba mali zangu zote zinazohamishika na zisizohamishika zitamilikiwa na mke/mume wangu aitwaye:

   ...............................................................

   Iwapo atakuwa hai baada ya kufa kwangu

6. Iwapo mke/mume wangu aitwaye:

   ...............................................................................

   Atafariki mapema kuliko mimi, mali zangu zitarithiwa na watoto wangu wafuatao:-

   a. ..............................................................
      S. L. P: ..............................................
      Simu: ..............................................

   b. ...............................................................
      S. L. P: ..............................................
      Simu: ..............................................

c. ..............................................................

S. L. P: ..............................................

Simu: ..............................................

d. ............................................................

S. L. P: ..............................................

Simu: ..............................................

e. ............................................................

S. L. P: ..............................................

Simu: ..............................................

f. ............................................................

S. L. P: ..............................................

Simu: ..............................................

g. ............................................................

S. L. P: ..............................................

Simu: ..............................................

h. ……………………………………………………
S. L. P: ………………………………………
Simu: …………………………………………

i. ……………………………………………………
S. L. P: ………………………………………
Simu: …………………………………………

Katika mafungu yaliyo sawa sawa imetiwa sahihi hapa…………………………………………………
siku ya………………………………………………
Mwezi wa…………………………………………
Mwaka………………………………………………

Sahihi ya kwanza
Jina: ……………………………………………………
Sahihi: ………………………………………………
Anuani: ……………………………………………
……………………………………………………………
Kazini: ………………………………………………
……………………………………………………………

Mbele ya:-

...................................................................................

...................................................................................

...................................................................................

Kamishna wa viapo/sahihi




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*